

## **Utangulizi**

Kitabu hiki ni uamsho wa fahamu na fikra zetu kama binadamu katika kuyatafakari mambo na kuyaelewa. Pengine kujivua gamba na ngozi ya ubinadamu wa kawaida tuliouzoa ama kukuzwa nao na kuzama ndani ya nafsi zetu kujitafuta zaidi ili kujijua. Kujijua kwetu ndiko kunakoyapa maisha yetu thamani.

Pasina kujijua hatuna tofauti na mfu, yaani; mwili usio na uhai. Ni kama chupa ya maji tupu tu! Chupa yenye maji ya kunywa, thamani yake ni yale maji yaliyo ndani ya chupa na si chupa iliyobeba maji. Hii ndiyo hasa dhima ya kitabu hiki.

Kitabu hiki kinaangazia thamani ya ubinadamu wetu kwa mtu mmoja mmoja. Pengine kuyatazama maisha katika pembe ya kimazingira na uhalisia. Kuyaelewa mazingira na uhalisia wake ndiko kunakoyapa maisha yetu mjongo kwa kuyaishi ipasavyo.

Lakini, unafikiri unaweza kumudu kuyaelewa, kuyaishi na kuyafurahia maisha pasina kujijua

wewe ni nani? Wewe ni chupa iliyobeba maji ama wewe ni maji yaliyopo ndani ya chupa?

Pengine ni rahisi kujibu kwa haraka kwa kuwa tunajua ni kipi chenye thamani kwa mfano huo! Lakini je, unajijua? Unajijua wewe ni wa thamani? wa thamani kiasi gani? Wa thamani kwa namna gani?

Basi kitabu hiki kinakufunulia ya sirini na bayana yatakayoanzisha kama si kukamilisha safari yako ya kujijua wewe ni nani!